

COMPETENCE BASED CURRICULUM

D003

MONITORING LEARNER'S PROGRESS

GREDI YA NNE - MWAKA 2022

[4]

KISWAHILI

Jina:

Nambari ya Mwanafunzi :

Jinsia: Mvulana Msichana

Jina la Shule:

Kuzidisha matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio

SEHEMU YA KWANZA : KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

(alama 5)

1. Mwalimu amwulize mwanafunzi maswali yafuatayo huku akilibu kwa usahihi

(a) Mahali ambapo shughuli za upishi hufanyika huitwaje?

(Mwanafunzi ajibu)

(b) Taja viungo viwili vya mapishi.

(Mwanafunzi ajibu)

(c) Vifaa gani vya kupikia vinapatikana jikoni mwenu?

(Mwanafunzi ajibu)

(d) Kijiti kinachotumiwa kusonga ugali huitwa?

(Mwanafunzi ajibu)

SEHEMU YA PILI : KUSOMA KWA SAUTI

(alama 10)

2. Soma habari ifuatayo kwa sauti huku mwalimu akisikiliza.

Mwalimu wa somo la Kiswahili katika gredi yetu anaitwa Rita. Yeye hufunza vizuri sana. Anapotufunza, huwa ninatifuraha somo lake. Juzi alitufunza kuhusu matumizi ya kamusi. Alianza kwa kutueleza kuwa kamusi ni kitabu cha maneno yaliyopangwa kwa utaratibu wa alfabeti. Alfabeti pia huitwa abjadi. Pia, alitueleza kuwa kamusi hutoa maana ya neno na maelezo mengine yanayolihusu neno hilo. Katika somo hilo, Bi. Fatuma alitufunza abjadi hizi za kiswahili; a, b, ch, d, e, e, f, g, h, i, j na nyingine nyingi.

SEHEMU YA TATU : SARUFI

1. **Andika wingi wa nonimo hizi.**

- (a) Sahani _____
(b) Zulia _____
(c) Ruinga _____

(alama 3)

2. **Ambatanisha maamkizi au maagano na majibu yake**

- (a) U hali gani binuru
(b) Alamsiki marahaba
(c) Shikamoo vyema
(d) Umeamkaje njema

(alama 4)

3. **Panga maneno haya jinsi yanavyofuatana katika kamusi.**
pakua, chumvi, nidhamu, agiza, meza

(alama 5)

- a) _____
b) _____
c) _____
d) _____
e) _____

4. **Tumia sifa zilizo mabanoni kujibu maswali.**


(alama 3)

(a)




Kikombe hiki ni _____
(chafu)

(b)



Huyu ni ndovu, ndovu huwa _____
(kubwa)

(c)



Miti hii ni _____
sana. (refu)

5. Unda maneno kwa kutumia silabi hizi. (alama 3)

- (a) da _____
(b) po _____
(c) ti _____

6. Tegua vitendawili vifuatavyo (alama 2)

- (a) Popote niendapo ananifuata _____
(b) Nyumba yangu haina mlango _____

SEHEMU YA NNE: UFAHAMU

(alama 5)

Soma ufahamu huu kisha ujibu mwaswali vafuatayo

Musa ni mzee mwenye bidii sana. Yeye hufanya kazi ya useremala. Katika karakana yake, yeye hutengeneza meza, makochi na vifaa vingine vya samani. Yeye hupenda kuvaa bwelasuti ili nguo zake zisiwe chafu. Pia huvaa chepeo ili kuzuia ukali na miale ya jua. Amejenga nyumba yake upande wa Kusini mwa shule ya Ajera. Nyumba hiyo ina vyumba kama vile sebule, msala, jikoni na chumba cha kulala.

Kila jioni, mzee Musa na familia yake ya watu saba, watoto wanne na mke mmoja, hukutana ili kula. Chakula hicho huwa kitamu kama halua. Kila mmoja hunawa kwa maji safi na sabuni kabla ya kula. Watoto husubiri wazazi wanawe kwanza ndipo nao wanawe. Kila mtu hula akiwa amenyamaza. Wanaelewa kuwa kuongea na chakula mdomoni ni tabia mbaya. Baada ya kula, wote hunawa. Watoto huondoa vyombo mezani kisha humsaidia mama yao kuviosha.

(a) Habari hii inaeleza kuwa mzee Musa hufanya kazi gani?

(b) Mzee Musa huvaa bwelasuti ili _____

(c) Familia ya mzee Musa ina watu wangapi?

(d) Chakula kinacholiwa na familia ya mzee Musa huwa kitamu kama

(e) Kwa nini familia ya mzee Musa hula kama imenyamaza?
